## Shule za Umma za Kaunti ya Fayette
## Mwongozo wa marejeo ya haraka kwa Vipawa na Vipaji - daraja la 4 hadi 12

KRS 157.230 inahitaji shule za wilaya kuendesha mipango ya watoto wa kipekee katika viwango vyote vya daraja. KRS 157.230 inaweka wanafunzi wenye vipawa chini ya kitengo cha "wanafunzi wenye kipaji maalumu" chini ya ufafanuzi wa "Watoto wa kipekee".

Mipango 704 KAR 3:285 ya wenye vipawa na vipaji, inahamuru kwamba wanafunzi watambuliwe kuwa wana thibitisha uwezo wa kufanya  vizuri katika kiwango cha juu kabisa katika hali ya kiakili, hali maalumu ya  kitaalum, katika fikra na mawazo tofauti, kisaikolojia au ujuzi wa uongozi, au katika sanaa au maonyesho. Wanafunzi wa shule ya msingi wanatakiwa kuchunguzwa na kuchaguliwa kama wanafunzi wenye uwezo mkubwa katika kundi la vipaji vya Msingi (Primary Talent Pool) (PTP). Na wanafunzi katika darasa 4-12 wanaweza kutambuliwa rasmi kwa huduma katika eneo moja au zaidi ya vipawa.

### Ufafanuzi wa Vipagji 704 KAR 3:285

Uwezo wa kiakili kwa ujumla : ni kuwa na uwezo au kuthidbitisha njia za kufanya jambo Fulani kwa kiwango cha juu kabisa katika ngazi ya kiakili na kuwa na uwezo zaidi wa akili kuliko watoto wa umri uzoefu, au mazingira mamoja kama yake. Uwezo wa kiakili kwa ujumla uonekana kwa kawaida katika utendaji wa ziada katika maeneo ya utambuzi, kama vile hoja isiyo dhahiri, ufahamu wa kijamii, kumbukumbu, uhusiano wa anga, uchambuzi, usanisi na tathmini ya habari.

Uwezo Maalum wa Kielimu:- ni kuwa na uwezo unaowezekana au kuthibitisha mamlaka ya  kufanya jambo katika kiwangi cha juu kabisa katika maeneo maalum ya kitaaluma kwa kiasi kikubwa zaidi ya umri, uzoefu au mazingira ya wenzake wa umri moja. Wakati wanafunzi walio na uwezo maalum wa kielimu kwa kawaida wanaangalau uwezo wa kielimu, mara nyingi wana uwezo mkubwa wa utendaji wa hali ya juu katika eneo moja au zaidi ya masomo yanayohusiana.

Uwezo wa Uongozi au wa Kisaikolojia: kuwa na chipukizo ya uwezo au kuthibitisha uwezo wa kipekee katika jambo kwa kiwango cha juu kabisa katika ustadi wa kijamii na sifa za utu kama vile utulivu, uwezo wa kusoma na kujieleza vizuri kwa masemi na maandishi, uwezo wa usimamizi, na uwezo, au maono ya kuweka malengo na kupanga na kuwaongoza wengine kufikia malengo hayo.

Uwezo wa Sanaa na kuigiza wa kuoneakana: ni kuwa na uwezo au kuonyesha uwezo wa kufanya jambo kwa kiwango cha juu kabisa katika sanaa na uigizaji na kuthibitisha au kukamilisha uwezo wa utengenezaji bora wa urembo, mafanikio au ubunifu katika maeneo kama sanaa, densi, mchezo wa kuigiza, usemi, na katika shughuli zinahitaji utumiaji wa kipekee wa misuli kubwa na ndogo za mwili.

Uwezo wa kufikiri na kubuni tofauti: ni kuwa au kuonyesha uwezo wa kutenda kitu kwa kiwango cha juu kabisa katika fikra za kubuni na njia tofauti za kazi za kawaida kama inavyothibitishwa na hoja ya ubunifu, ufahamu wa hali ya juu na mawazo, na kutatua shida kwa njia za kipekee.

### Uchunguzi wa Vipaji na Vipawa 4-12

Kwa kawaida, Wilaya huwatambua rasmi wanafunzi katika darasa la nne hadi kumi na mbili ( 4-12) ili washiriki katika huduma za vipaji na vipawa. Kwa kufuata sheria zinazotumika na kanuni za kiutawala, Wilaya itatoa chaguzi kadhaa zinazofaa za huduma katika mazingira ambayo hushughulikia uwezo,  maslahi na mahitaji ya wanafunzi wanaostahiki huduma katika kundi moja (1) au nyingi zifuatazo: uwezo wa kiakili kwa jumla; ustadi maalum wa kitaaluma; mawazo ya ubunifu au tofauti; ujuzi wa kisaikolojia au kiuongozi; na sanaa za maonyesho.

Upimaji wa kiakili wa jumla- upimaji wa akili wa kitaalam kwa ujumla hufanyika katika Kaunti mzima kila mwaka kwa wanafunzi wote wa darasa la 3 kupitia Mtihani wa Uwezo wa utambuzi.

Upimaji maalum wa kitaaluma: - Upimaji kwa Kaunti mzima hufanyika kila mwaka kwa wanafunzi wote wa darasa la 3 katika elimu ya kusoma, hisabati, sayansi na masomo ya kijamii.

Ubunifu: uchunguzi wa Kaunti mzima hunafanyika kila mwaka kwa wanafunzi wote wa darasa la 4 kupitia chombo cha ubunifu.

Uongozi: - uchunguzi wa Kaunit mzima hufanyika kila mwaka kwa wanafunzi wote wa darasa la 4 kwa kutumia Utafiti wa Uongozi wa Wenzio.

Sanaa za kuonesha na kuigiza: ukaguzi wa sanaa na maonyesho na maigizo hufanyika kwa wanafunzi wa darasa la 4 wanaovutiwa. Wazazi wote watapokea barua ya taarifa.

*Kumbuka : Daraja zingine zote huchunguzwa kila mwaka kupitia pendekezo, data ya matokeo na maendeleo, na/au sosiogramu. Fursa zingine za upimaji zinaweza kutokea katika mwaka kwa sababu ya mazingatio maalum na mazingira kulingana na rufaa ya kipekee ya wanafunzi na/au ulemavu.*

## Hatua rasmi za Utambulisho wa vipawa 4-12

1) Kutokana na upimaji, uchunguzi au pendekezo, walimu watakusanya ushahidi unaohitajika kwa kila eneo. Pendekezo za wenye vipawa zinaweza kufanywa na wazazi, walimu, wanafunzi, wafanyakazi wengine wa shule. Mwanafunzi lazima awe na angalau hatua tatu(3) halali za zinazokubalika kwa kila kategoria ya vipawa ili kutambua nguvu na tabia zenye vipawa ambazo zinaonyesha uhitaji na ustahiki wa chaguzi za huduma. Mwalimu mwenye rasilimali ya vipawa anawezesha michakato yote ya uchunguzi na kutambulisha.

2) Wanafunzi lazima wapate alama 9 ya stanine score ya kiwango kamili cha kawaida ya kipimo cha akili katika eneo ya akili kwa jumla. Katika maeneo Maalum ya Utalaam, wanafunzi lazima wapate alama za ujumuishaji 9 ya stanine score kwenye jaribio la mafanikio ya marekebisho yaliyowekwa sanifu kwa kila eneo maalum la taalamu. Wanafunzi lazima pia wawe na angalau vipande viwili vya ushahidi halali kwa kila eneo.

    - Ushahidi wa uongozi lazima ujumuishe utayari au ushiriki wa uongozi katika darasa, shule na jamii.
    - Ushahidi wa sanaa ya maonyesho lazima uwe pamoja na utendaji, au mapendekezo na kwingineko.
    - Ushahidi wa ubunifu lazima uonyeshe uwezo wa kufikiria wa ubunifu.

3) *Kamati ya Mapendekezo ya Vipaji (Gifted Recommendation committee – GRC) itakutana kuchambua data zote na ushahidi ili kufanya maamuzi kuhusu chaguzi zinazowezekana za upimaji, utambulisho/uwekaji wenye vipawa, na huduma zinazopaswa kutolewa. Wanachama ni, ila sio tu, wafanyakazi wenye vipawa, walimu wa darasa na eneo maalum, utawala, washauri, walimu wa elimu maalum, walimu wa EL, na wafanyakazi wowote ambao wanotambua rasmi na kuamua uwekaji wa wanafunzi kupitia sera za Wilaya. Mikutano ya utambuzi wa vipawa vipya na upimaji itafanyika wakati baridi na/au masika.*
   *KUMBUKA: Wazazi/Walezi wanaweza kuwasilisha malalamiko yao ya utambulisho na/au chaguzi za huduma kwa kukamilisha orodha ya Chumba cha Uchunguzi na Malalamiko. Wazazi wanaweza kuomba waraka hii ya malalamiko kutoka kwa mwalimu wa raslimali ya*

*vipawa au Ofisi ya Vipaji na Vipawa ya Wilaya. Kamati ya Malalamiko Kuhusu vipawa na vipaji ya Wilaya itafanya maamuzi yote ya mwisho juu ya malalamiko.*

**Ili kuhakikisha taratibu sawa za uchunguzi na utambulisho kwa wanafunzi ambao hawajawakilisha kijadi (ulemavu wa kipekee, vikundi vya rangi/kabila ambavyo havikufaidika, wanafunzi wa kiingereza, na wake wasiofaulu) katika elimu ya vipawa na vipaji, taratibu bora za mazoezi zitatumika kutambua wanafunzi wanaostahiki huduma zenye vipawa na vipaji kupitia mazingatio maalum.**

## Muhtasari wa Utoaji wa Huduma kwa Wanafunzi wenye vipawa waliotambuliwa rasmi 4-12

Kulingana na 704 KAR 3:285 shule itatofautisha, kubadilisha, kurekebisha au kugeuza mitaala kuwezesha kufikia kiwango cha juu cha malengo ya kujifunza yaliyoanzishwa katika KRS 158.6451 na kusaidia wanafunzi waliotambuliwa na kugundulika kama wenye vipawa na wenye vipaji vya kukuza zaidi masilahi yao, mahiataji na uwezo .

Kuptiia njia za kushirikiana, shule itaandaa chaguzi za utoaji wa huduma ambazo zinalingana na mahitaji, nia na uwezo maalum ya mwanafunzi. Muhula wa kwanza wa kila mwaka wa shule, kamati itakutana kuamua chaguzi zinazofaa za utoaji wa huduma kwa kila mwanafunzi. Walimu wa rasilimali ya vipawa watasaidia utoaji wa huduma kupitia angalao chaguzi mbili za chini. Chaguzi za huduma zinaweza kuwa mchanganyiko wa, na zaidi ya, utofautishaji, utajiri, kuongeza kasi, ushirkiano, na mashauriano.

Baada ya utambulisho wa awali, na kila mwaka wakati wa masika, wanafunzi wenye vipawa watapokea Mpango wa Huduma wa Wanafunzi wenye vipaji. Na tena, kila mwisho wa muhula, Ripoti ya Maendeleo ya Mpango wa Huduma ya Wanafunzi wenye Vipaji itapatikana shuleni.

**Shule zinajukumu la kutoa utofautishaji unaofaa kwa wanafunzi wote bila kujali kiwango cha uwezo wao au ikiwa utambulisho maalum wa vipaji umefanywa.**

## Chaguzi Maalum za Utoaji wa Huduma kwa Wanafunzi wenye Vipaji 4-12

Vikundi vya madhumuni ya kufundisha na chaguzi nyingi za utoaji huduma zitatumika katika mpango wa elimu wenye vipaji wa wilaya. Muundo wa kupanga wanafunzi utajumuisha vikundi kwa madhumuni ya kufundisha kulingana na masilahi ya mwanafunzi, uwezo na mahitaji, kama vile ya kijamii na kihisia.

Kutakuwa na chaguzi nyingi za utoaji huduma bila chaguo moja ya huduma iliyopo peke yake, katika wilaya na kwa kiwango cha daraja. Chaguzi hizi za utoaji wa huduma zitatofautishwa kwa kiwango kinacho lingana na KRS 157.200(1). Vikundi vyote viwili kwa madhumuni ya kufundisha na chaguzi nyingi za utoaji huduma kama vile:

- Chaguzi tofauti za kuharakisha ( kwa mfano, kutoka mapema masomo ya msingi, kuruka daraja, kuruka yaliyo na mtaala katika elimu moja (1) au zaidi katika kiwango cha daraja la juu).
- Mafundisho ya kushirikiana
- Huduma za ushauri
- Huduma za Rasilimali
- Huduma maalum za ushauri
- Kujifunza kwa umbali
- Utafiti wa kujitegemea
- Semina
- Uzoefu tofauti za masomo kwa watu binafsi na vikundi vya nguzo katika darasa la kawaida.

- Huduma za kujitajirisha wakati wa siku ya shule (lazima zifanyike wakati wa siku ya shule, hakuna masomo ya ziada);
- Ushauri
- Darasa la heshima
- Kurushwa kwa ngazi ya juu
- Uwekezaji wa hali ya juu
- Chaguzi za masomo ya kusafiri
- Shule maalum au madarasa yenye kujitegemea, kuanza darasa la nne (4) hadi darasa la kumi na mbili (12) tu.

## Usawazishaji wa utambulisho

Usawazishaji hutolewa kwa utambulisho wenye vipawa ambao unatokea katika Shule za Umma za Wilaya ya Kentucky. Mfumo wa kampasi huhamisha rekodi zote zilizo na vipawa (vipaji) kutoka wilaya moja hadi nyingine. Chaguzi za utoaji wa huduma zinakaguliwa katika wialya mpya na kurekodiwa katika Mpango wa Huduma ya Wanafunzi Wenye Vipaji. Wanafunzi ambao huhamia kutoka jimbo linguine au shule ya binafsi/shule ya nyumbani hawajapewa usawazishaji na lazima wapimwe kulingana na kanuni za Vipaji ya Kentucky. Shule zitapitia alama za mtihani zilizokadiriwa za mwanafunzi na ushahidi wa ziada. Pia, ushahidi wa ziada unaohitajika unaweza kukusanywa pamoja na usimamizi unaowezekana wa tathmini zilizoainishwa kwa kawaida.